

# Watu Mazingira

## *Ulimwengu!*


Toleo la 3/Julai-Septemba 2018

**Kwa Mapenzi ya Ndege**

**Mbinu Asili za Uhifadhi wa  
Bio-Anuai Sehemu Kame**

**Changamoto za Kuweka  
Kumbukumbu za Elimu ya  
Jadi**

**Upanzi wa Miti Shambani  
ni Kilimo Mbadala!**



## Yaliyomo



## Taarifa kutoka Kamati Kuu

3

Kamati kuu yatoa mtazamo wake kuhusu maendeleo na ufanisi wa Watu Mazingira Ulimwenguni katika robo ya tatu.

## Kwa Mapenzi ya Ndege

4

Kutana naye Joseph Chekangor, mpenda ndege na mpiga picha.

## Mbinu Asili za Uhifadhi wa Bio-anuai Sehemu Kame

6

Mama Ziro asimulia juhudi zake za kuregesha upya misitu asili ya Pwani, Kaunti ya Kilifi, Kenya.

## Changamoto za Kuweka Kumbukumbu za Elimu ya Jadi

8

Jazzy Rasolojaona aeleza changamoto za mchakato wa kuunda mikakati ya jamii ya matumizi ya bio-Anuai.

## Miti Shambani ni Kilimo Muafaka!

11

Nancy Saumu Ronald apendekeza vijishamba vya miti shambani kukimu mahitaji ya mbao.

## Mseto wa Habari!

13

Habari za hapa na pale kuhusu wanachama wetu zilizotufikia.

KAMATI KUU

Silvanus Uunona – Mwenyekiti,

Yaa Tiwah – Mwenyekiti Mwenza,

Moses Ziro – Katibu,

Frank Maro – Mweka Hazina,

Phathisani Tabengwa – Mwanakamati,

Cheli Gurung – Mwanakamati,

Nancy Saumu Ronald – Mwanakamati,

Emma Kyomukama – Mwanakamati.

MAJUKWAAJukwaa la Maji na Maeneo Lowevu

Mshirikishi: Silvanus Uunona (Namibia),

Mshirikishi Mwenza: Soledad Castro (Costa Rica).

Jukwaa la Misitu na Wanyama Pori

Mshirikishi: Nancy Saumu Ronald (Kenya),

Mshirikishi Mwenza: Dorothy Syallow (Kenya).

Jukwaa la Kilimo Hifadhi na Uvuvi

Mshirikishi: Yaa Tiwah (Ghana),

Mshirikishi Mwenza: Setondji Gaston (Gabon).

Jukwaa la Elimu na Hamasisho

Mshirikishi: Phathisani Tabengwa (Zimbabwe),

Mshirikishi Mwenza: Zelalem Abera (Ethiopia).

Jukwaa la Vijana

Mshirikishi: Cheli Gurung (Nepal),

Mshirikishi Mwenza: Raymond Mwambire (Kenya).

Jukwaa la Jamii Asili

Mshirikishi: Emma Kyomukama (Uganda),

Mshirikishi Mwenza: Michael Wamalwa (Tanzania).

Jukwaa la Biashara Endelevu za Mazingira

Mshirikishi: Frank Maro (Tanzania),

Mshirikishi Mwenza: Fadhila Ghikas (Kenya).




# Taarifa ya Kamati Kuu

Tumekamilisha shughuli za robo ya tatu ya 2018. Shughuli nyingi katika robo hii zilifanyika katika majukwaa yetu.

Kulikuwa na mjadala kadhaa, na kati ya mjadala uliosisimua ni ule wa Kuundwa kwa Mtandao wa Kina Mama chini ya Jukwaa la Elimu na Hamasisho. Mjadala huu ulikuwepo 2017 lakini haukupata kuungwa mkono kikamilifu. Hata hivyo, wakina mama mashinani walifufua mjadala huu na kuweza kuungwa mkono na wakina mama wengi. Mtandao huu, kulingana na kina mama, utalenga kujenga uwezo wa akina mama kuweza kuhusika kikamilifu na kunufaika kutokana na usimamizi bora wa mazingira. Kamati itaangalia mapendekezo na maoni yaliyotolewa na kutoa muelekeo.

Jukwaa la misitu na Wanyama Pori lilikuwa na mjadala tata kuhusu matumizi ya wanyama pori na misitu. Ikumbukwe kwamba kulikuwa na Jopo Kazi lililoundwa na Wizara ya Utalii na Wanyama Pori kutathmini mbinu bora ya kutekeleza matumizi haya. Wanachama katika jukwaa walikuwa na tashwishwi kuhusu utekelezaji wake kwa vile wengi waliiona kama mbinu ya kuhalalisha uwindaji haramu wa wanyama pori. Na badala yake, wanachama walipendekeza kuimarishwa kwa miundo misingi ya ufugaji kama njia mbadala ya kuinua mapato na lishe. Njia hii pia ilionekana kuambatana na tamaduni za jamii mashinani.



Sera na muongozo wa kulinda watoto iliundwa na Jukwaa la Vijana kipindi hiki. Muongozo huu unaangazia kujitolea kwa Watu Mazingira kulinda haki za watoto ndani ya mtandao na pia watoto ambao huenda wakaathiriwa moja kwa moja ama kwa njia nyingine kutokana na shughuli za mtandao wa Watu Mazingira. Muongozo huu utajadiliwa na kupitishwa kabla mwisho wa mwaka 2018.

Ni vigumu kupuuza athari za mabadiliko ya hali ya hewa. Jukwaa la Kilimo Hifadhi na Uvuvi waliliangazia jambo hili kwa vile wakulima na wavuvi wengi wameathirika. Kuna mapendekezo kadhaa yaliyotolewa kukabiliana na hali hii. Kuna haja ya kuwa na mseto wa mbinu za kuwasaidia wakulima na wavuvi, hasa usaidizi wa wataalam katika uzalishaji, fedha na masoko.

Mtandao wa Watu Mazingira umekuwa ukisaidia juhudi za upanzi wa matumbawe kisiwani Wasini, Kenya. Jukwaa la Maji liliweza kupokea taarifa ya jinsi bustani za matumbawe huanzishwa na kukuzwa ili kuregesha upya sehemu

zilizoharibiwa za matumbawe.

Mjadala muingine uliosisimua ni ule wa Jukwaa la Jamii Asili. Jukwaa lilijadili jinsi ya kusaidia jamii mashinani kufaidi kutokana na biashara ya chembechembe za rasili mali za biolojia. Bwana Jazzy Razalojaona amelivulia njunga jambo hili na kutupa taarifa ya mtazamo wake kuhusu changamoto za kuanzisha biashara hii nchini Madagascar.

Majukwaa yote yalijizatiti kujiandaa kwa shughuli za kufunga mwaka kwa kutayarisha mikakati ya kuchagua waliobobea katika kuboresha mazingira yetu na kuchangia malengo ya Watu Mazingira. Jukwaa la Vijana walipendekeza vijana wenye talanta za kuchora, kuimba na kuandika tamthilia za mazingira waweze kutuzwa. Jukwaa la Biashara wakapendekeza vijana wanaowekeza mara kwa mara katika akaunti zao pia waweze kutuzwa tuzo la Hazina Mazingira.


Hatimaye, Jukwaa la Elimu na Hamasisho lilipendekeza kutuza tuzo la Balozi wa Mazingira kwa wale waliosaidia kukusanya rasilimali kwa shughuli na miradi ya Watu Mazingira; kuhamasisha jamii kuhusu shughuli za Watu mazingira; kuchangia kutengeneza habari za uhamasisho; na kuandikisha wanachama zaidi. Hii ni mbali na kuandikisha familia zao ambao watatuzwa tuzo la Familia.

Ahsanteni!



# Kwa Mapenzi ya Ndege

Kutana na Joseph Chekangor, mpenda ndege na mpiga picha hodari.



Ziwa la Baringo limeanza kuwa maarufu kwa watalii. Hii imechangiwa pa kubwa na aina 470 ya ndege wanaopatikana hapa.

Ziwa Baringo linapatikana Kaunti ya Baringo nchini Kenya na ina ukubwa wa kilomita 130 mraba. Ziwa hili lina visiwa 13 na ni moja ya ziwa lenye maji tamu katika bonde la ufa. Mzungu wa kwanza kufika hapa alikuwa Joseph Thomson mwaka wa 1883 na hapa pia ndipo mwana jiolojia Prof. John Walter Gregory aliweza kueleza jinsi Bonde la Ufa lilivyoundwa kutokana na uchunguzi wa ziwa hili mwaka wa 1892.

Katika kituo cha biashara cha Kambi ya Samaki, kando kando ya ziwa Baringo, tunakutana na Joseph Chekangor. Joseph ni mpenda ndege na hamu ya kujua zaidi kuhusu ndege imekuwa tangu 2005.

Joseph alikutana na Terry Stephenson, mtaalam wa ndege, mwaka wa 2005 na kumpa motisha wa kupenda ndege na kupiga picha. Terry anashikilia rekodi ya dunia ya kuweza kurekozi ndege wengi zaidi ndani ya masaa 24 ya ndege 342.

Kuwepo kwa ndege wengi, wakiwemo wakaazi na pia ndege wa kuhama hama, uliwezesha ziwa Baringo kutambulika kama Eneo Muhimu la Ndege. Kati ya ndege wanaopatikana hapa ni kama vile mbuni, tai, bundi na aina nyingi za ndege wa maji.

Joseph Chekangor hakuwa peke yake mwenye hamu ya kujua na kupenda ndege. Rafiki yake Francis Cherotich aliungana naye kuunda Kikundi cha Uhifadhi wa Bio-Anuai ya Ziwa



Baringo mwaka wa 2007, wakijumuisha wenzao kumi na wawili. Kupitia juhudi za kikundi hiki, ndege na makazi yao katika ziwa Baringo zimeweza kuhifadhiwa.

Mbali na juhudi za kuhifadhi ndege na makazi yao, Joseph alitaka sana kurudi shule kuongeza elimu na ujuzi wake. Si ajabu Joseph alijiunga na Taasisi ya Mafunzo ya Wanyama Pori Kenya kule Naivasha mwaka wa 2014. Hata hivyo, juhudi za Joseph kumaliza masomo yake zilikatizwa alipokosa karo.


Je jambo hili lilikatiza juhudi na ndoto ya Joseph kuhusu ndege? La hasha! Joseph alirudi nyumbani na kuendeleza kazi za kikundi chao cha Uhifadhi wa Bio-anuai ya Ziwa Baringo. Hatimaye juhudi zake za kutaka kujua kupiga picha kama mtaalam zilionekana na kumpendeza mmoja wa watalii waliokuwa wametembelea ziwa Baringo. Mgeni huyu ambaye Joseph alikuwa akimtembeza alimpatia kamera ya wapiga picha za kitaalam. Kamera hii ilifungua milango zaidi kwa Joseph ya kuweza kukutana na wapiga picha za kitaalam.

Kikundi cha Uhifadhi wa Bio-anuai ya Ziwa Baringo kilipigwa jeki mwaka huu pale Nature Kenya walipoanzisha kuhesabu ndege wa maeneo lowevu katika ziwa Baringo Juni 2018. Kati ya watu maarufu waliohudhuria shughuli hii ni Fleur Ng'eno, mpenda ndege na mwanachama wa Nature Kenya na Rupi Mangat, mwandishi wa habari za mazingira na utalii.

Kuna kila ishara kuwa ziwa Baringo litazidi kuwa eneo muhimu kwa watalii wapenda ndege. Joseph na wenzake wanaamini kuwa watakuwa wadau muhimu watakaochangia ziwa Baringo kuzidi kuwa kivutio kikubwa cha watalii.



Ndege aina ya Heuglin Courser anapendeza sana hasa kwa mtandao mweupe katika shingo yake. Joseph amempenda sana ndege huyu.



Nembo ya kikundi ambacho Joseph na rafikiye Francis Cherotich walianzisha.



# Mbinu Asili za Uhifadhi wa Bio-Anuai Sehemu Kame

Mama Ziro (kushoto) asimulia juhudi zake za kuregesha upya misitu asili ya Pwani, Kaunti ya Kilifi, Kenya.

Mara ya kwanza Mama Constance Ziro kufika Kayafungo, Kaunti Ndogo ya Kaloleni, Kaunti ya Kilifi, Kenya, ilikuwa miaka ya awali ya 1970. Alipowasili, sehemu nyingi zilikuwa ni msitu. Na mara nyingi alitembea Kayafungo nyakati za Krisimasi, wakati familia yote ya bwanake ilikusanyika kwa sherehe hizo.

Safari za mara kwa mara kuja Kayafungo zilifika ukingoni 1981 alipoamua kuhamia huko. Alipokuwa akitengeneza makao ya kudumu huko, alitamani sana kutengeneza mji kwa mfano wa mji wa mama Luweti (Lily White), mjini Kilifi. Kwa kuiga makao ya Luweti, alipanda maua mengi na alikuwa wa kwanza kijijini kupanda mboganzila.

Alipowasili alijitosa katika kilimo mseto, akipanda mimea kadha wa kadha na ufugaji. Kati ya mimea aliyokuza ni mahindi, njugu, kunde, mtama, vitunguu na nyanya. Aliweza kufuga kuku, mbuzi, ngombe za kienyeji na ngombe za kisasa kutoka Ulaya.

Mama Ziro alinenda kuiumuika

katika shughuli za maendeleo ya jamii, hasa vioto vya kujenga uwezo wa wanawake mashinani nchini Kenya. Kupitia kwa juhudi zake na za wakina mama 31 wapenda maendeleo, waliweza kuunda kikundi cha wakina mama cha Lamukani (Amkeni!) mwaka wa 1983. Alikuwa mwenyekiti wake wa kwanza na kufikia 1989, aliweza kuchaguliwa Katibu wa Maendeleo ya Wanawake wa Wilaya ya Kilifi. Kwa ushawishi wake ma wenzake, aliweza kuleta pamoja vikundi 200 vyenye jumla ya wanachama 6000 kuunda Muungano wa Vikundi vya kina Mama Kaloleni. Juhudi zake za maendeleo ya kina mama zilizawadiwa wakati alipoteuliwa Diwani Maalum katika Baraza za Madiwani, Kaunti ya Kilifi mwaka wa 1998.

Muungano wa kina Mama wa Kaloleni waliweza kupata ufadhili kutoka kwa Hazina ya Kimataifa ya Mazingira kupitia Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa. Kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Egerton,

waliweza kutekeleza mradi wa uhifadhi wa bio-anuai

ya maeneo kavu. Kati ya kazi mradi walizotekeleza ilikuwa upanzi wa miti na ujenzi wa mabwawa. Kupitia kwa mradi, Mama Ziro aliweza kupanua bwawa shambani mwake lakini hakufaulu katika upanzi wa miti.

Kwa miaka mingi, Mama Ziro aliweza kutafiti na kutambua njia muafaka ya kukuza miti katika maeneo kavu. Baada ya kujaribu kilimo cha mfumo wa kuhama hama, Mama Ziro alitenga eka 7 maalum kwa kilimo na ufugaji. Sehemu iliyobaki ya zaidi ya ekari 30 iliwachwa tu hivyo. Bila usumbufu kutoka kwa mifugo ama kilimo cha mimea, miti



Shamba la mahindi lililozungukwa na msitu.



iliweza kukuwa upya na kujaza sehemu zilizokuwa wazi.

Mama Ziro alikuwa na filozofia rahisi ya kukuza miti. Aliamini kuwa ardhi ikiwachwa bila usumbufu itaweza kuregesha miti na msitu unaofaa sehemu ile. Alikuwa amejaribu awali kupanda na kukuza miti bila kufaulu. Mingi ya miti aliyopanda ilikufa kutokana na ukame, kuibwa ama kuharibiwa na mifugo. Kwa kuacha ardhi bila usumbufu, aliwezesha mazingira kuchagua aina ya miti iliyofaa na kuikua bila ya kunyunyizia maji ama oparesheni nyingine za kukuza miti.

Kazi kubwa aliyoweza kufanya ni kuhakikisha kuwa eneo lililotengwa kwa miti halikuwa na usumbufu wa aina yoyote. Alifanya hivi kwa kuweka uzio, kuhakikisha barabara za watu zilizopitia shambani zilitafutiwa sehemu mbadala za kupitia na kupunguza mifugo wake. Alichukuwa hatua zaidi na kukomesha ukusanyaji wa kuni kwa sababu wengi wa wakusanyaji wa kuni walikuwa wakikata miti na kuicha ikauke ili waweze kuja kukusanya wakati mwingine wakirudi.

Kwa sasa shamba la Mama Ziro lina moja ya misitu asili ya Pwani iliyobaki katika Kaunti Ndogo ya Kaloleni, mbali na ule msitu wa Kaya Fungo. Wengi wnatambua nyumbani kwa Mama Ziro kama 'Kwa Ziro Msituni'.

Watafiti na waganga wa miti shamba wamevutiwa na aina ya miti ndani ya msitu huu. Kutokana na mvuto huu, Mama Ziro ameanza kuweka kumbukumbu za aina ya miti katika msitu wake. Kufikia sasa ameweza kutambua aina 62 ya miti asili na anakisia kuwa kuna zaidi ya miti 200 asili katika

shamba lake. Kufikia mwisho wa mwaka anaamini atakuwa amemaliza kuweka kumbukumbu ya miti yote.

Baadhi ya miti ambayo ameweza kuitambua ni kama vile mpingo (African ironwood; *Dalbergia*

kienyeji za mahindi ambazo zinastahimili ukame, hali ya udongo, pamoja na magonjwa na wadudu. Kwa sasa ameweza kukuza hifadhi ya mbegu za mahindi kama vile mdzihana (mahindi meusi), kanjerenjere (mahindi manjano), mbondeni



Mkingiri, *Dichrostachys Cinerea*

*melanoxylon*), ambao umeorodheshwa kama moja ya miti iliyo katika hatari ya kuangamia, kikwata (honey acacia; *Acacia mellifera*), mrihi (zebrawood; *Bracystegia spiciformis*), mbambakofi (lucky bean tree; *Azelia quanzensis*), mkingiri (marabou thorn; *Dichrostachys cinerea*), mbarao (red pod; *Terminalia brownie*), mvule (African teak; *Milicia excelsa*), mukowe (melia; *Melia volkensii*) na mkwaju (tamarind *Tamarindus indica*).

Mama Ziro pia amejaribu kuhifadhi mimea na mboga za kitamaduni. Baada ya kujaribu mbegu za dukani, Mama Ziro aliamua kujaribu mbegu za

(mahindi yenye majani meusi), mingawa (mahindi meupe) na mwangongo (mahindi mekundu). Mboga za kienyeji pia zinakua katika shamba lake kama vile mtsunga (*Launaea cornuta*), vongonya (*Asystacia gangetica*), logatsi (*Amaranthus graecizans*), mnavu (*Solanum spp*), kiswenya (*Amaranthus*) na kidemu (*Psilotrichum sericeum*).

Safari ya Mama Ziro katika uhifadhi imekuwa ya jitihada na kustahimili. Ni dhahiri kuwa juhudu zetu binafsi na jamii kwa ujumla zinaweza kuchangia pa kubwa katika uhifadhi ikiwa tutaheshimu mazingira yetu. Mchango huu hufaidi binadamu na mazingira kwa ujumla.

# Changamoto za Kuweka Kumbukumbu za Elimu ya Jadi

**Bw. Jazy Rasolojaona, Afisa, Natural Justice, Madagascar, aeleza changamoto za mchakato wa kuunda Itifaki ya Jamii ya matumizi ya bio-anuai.**

Tangu Umoja wa Mataifa, kupitia Mkataba wa Bio-Anuai kupitisha kipengele cha 8j, kumekuwa na mjadala hai kuhusu elimu tamaduni. Thamani ya elimu tamaduni ni kubwa na inahitaji kulindwa kwa vile inachangia uhifadhi wa bio-anuai. Watafiti na mashirika ya maendeleo pia wamevutiwa na mada hii. Kwa kweli, elimu tamaduni ni kielelezo cha rasilimali tunazomiliki na kwa sababu hivyo kulinda elimu hii ni muhimu kwa njia nyingi.



Bw. Jazy (kushoto mstari wa nyuma) asaidia jamii mashinani kuunda Itifaki ya Jamii ya matumizi ya rasilimali na elimu tamaduni.

Kwa upande mmoja, kulinda elimu tamaduni kuna hakikisha bio-anuai inayohusishwa na elimu hii inalindwa pia. Kutokana na ulinzi huu, kuna mjadala wa kufufua ama kuimarisha elimu hii. Ili kufaulu kufufua ama kuimarisha elimu hii, wamiliki wa elimu hii hushirikiana na watafiti ili wathamini elimu hii na waweze kugawa faida kwa makubaliano ya awali kati yao na washiriki wao. Mpangilio huu huanzishwa

na jamii kama hatua za mapema za kujilinda katika ushirikiano na washirika.

Kwa upande mwingine, wanaohitaji kutumia elimu tamaduni sharti mwanzo waombe na kupata ruhusa kutoka kwa wenye elimu hii. Mpango huu unalenga kulinda wenye elimu kutokana na walaghai ambao wanaweza kutumia vibaya elimu tamaduni kwa manufaa yao na

kuathiri wamiliki wa elimu na jamii kwa ujumla kwa kuwanyima faida itikanayo na elimu hii.

Njia hizi mbili ni tofauti. Lakini njia hizi mbili zimezua hoja ya vile zinatekelezwa na uhakiki wao wa kulinda elimu tamaduni. Ili kuhakikisha elimu tamaduni na wamiliki wa elimu hii wanalindwa, kuna haja ya kuwa na hifadhi ya





## Kipengele cha 8(j) – Elimu Tamaduni, Uvumbuzi na Matumizi

Kila upande wa wanao ingia katika mkataba ni sharti, kwa njia yoyote ile ambao inawezekana na sahihi: Kulingana na sheria za kitaifa, kwa kuheshimu, kuhifadhi na kudumisha elimu, uvumbuzi na matumizi ya jamii asili na jamii mashinani, kufuatia utamaduni unaowezesha uhifadhi na matumizi endelevu ya bio-anuai na kukuza matumizi yake kwa makubaliano na ushirikiano na wamiliki wa elimu, wavumbuzi na matumizi yake, na kwa kuhimiza ugavi sawa na wa haki wa faida za matumizi ya elimu, uvumbuzi na matumizi ya rasili mali za biolojia.

elimu tamaduni. Kupitia mpangilio huu, rekodi za elimu tamaduni zinahifadhiwa. Kulingana na Shirika la kimataifa la Mali Miliki (WIPO, 2016), uwekaji kumbukumbu za elimu tamaduni unahitaji makubaliano, shughuli za kupanga na kuratibu elimu hii ili kuwezesha kuinakili kwa njia ifaayo kwa kupitia rekodi, kidigitali ama kwa maktaba. Kwa njia hii, elimu tamaduni inaweza kuhifadhiwa kwa kuruhusu walio na idhini kuitumia na pia kuwezesha Ofisi za Mali Miliki kutoa vibali vya umiliki kwa wamiliki.

Mwaka huu, tumekuwa na mikutano kwa lengo la kunakili elimu tamaduni katika maeneo matatu nchini Madagascar. Maeneo haya ni (i) Jamii zinazosimamia mali asili Mariano, (ii) Wakulima wa Analavory na (iii) Wakulima wa Antavolobe. Mikutano hii ilikuwa moja ya shughuli za mchakato wa kumaliza Itifaki ya Jamii kuhusu Ufikiaji na Ugavi wa Faida zitokanazo na Chembechembe za Bio-Anuai. Mikutano hii ilipangwa na kuendeshwa na Bw. Jazzy. Kutokana na mikutano hii, Bw. Jazzy ana kubaliana na wale wenye mawazo kuwa uwekaji wa kumbukumbu za elimu tamaduni una umuhimu wake na mapungufu yake pia.

Kuweza kutambua elimu tamaduni kuna manufaa ya kuweza kulinda elimu hii kwa kuepuka kuipoteza, kwa vile kuna uzito unaopewa sayansi kuliko elimu tamaduni hasa na vijana siku hizi. Hata hivyo, jambo hili linategemea jamii husika. Kuna jamii ambazo hata waleo bado wanathamini elimu hii na ni rahisi kuweza kuitambua na kuihifadhi.

Kuweka kumbukumbu za ujuzi simulizi ni muhimu kwa vizazi vijavyo. Elimu ya kisasa imetulazimu kuweka kumbukumbu kwa maandishi. Mchakato wa kuweka kumbukumbu unaanza na kutambua wenye elimu na aina ya elimu tamaduni katika jamii. Kutokana na mchakato huu, kuna changamoto mbili. Ya kwanza, kukusanya elimu tamaduni ni kazi kubwa na inaweza kuwa ngumu kutegemea ukubwa wa jamii yenyewe na upana wa elimu tamaduni waliyo nayo. Kufaulu kunakili kumbukumbu hizi, kwa jamii zilizo tayari kufanya hivyo, mara nyingi hutegemea usaidizi wa kiufundi na fedha kutoka kwa washirika.

Pili, kunakili elimu hii kunahitaji kuangalia upya na kunakili elimu mpya mara kwa mara, kwa vile elimu pia hukua na kuongezeka. Jamii huvumbua elimu mpya mara kwa mara. Kwa sababu hii, kumbukumbu zao pia zinahitaji kuangaliwa mara kwa mara ili kwenda sambamba na ongezeko la elimu ndani ya jamii.

Tatu, kuweka kumbukumbu kuna hakikisha elimu hii inalindwa. Ni vigumu kuepuka matumizi mabaya ya elimu tamaduni, hasa elimu simulizi, ikiwa haija nakiliwa. Rekodi hizi zina ashiria uwepo wa elimu hii na wamiliki wa elimu ndani ya jamii. Je tunaweza kusema ni nani katika jamii ni mmiliki wa elimu hii? Tunawezaje kutambua watapeli? Kwa hivyo, ni muhimu kwanza utambuzi wa wamiliki wa elimu tamaduni kuwekwa bayana katika sheria ya

## Itifaki ya Nagoya

Itifaki ya Nagoya, kuhusu ufikiaji wa chembechembe za biolojia na ugavi wa haki na sawa wa faida zitokanazo na matumizi yake, wa Mkataba wa Bio-Anuai, ni mkataba wa kimataifa unaolenga ugavi wa faida kutoka kwa matumizi ya chembechembe hai kwa njia iliyo sawa na haki.



Itifaki ya Jamii ni mkusanyiko wa mikakati na masharti inayo paswa kufuatwa na serikali, makampuni na mashirika wanapo shirikiana na jamii mashinani kufikia na kutumia rasili mali na elimu tamaduni zao.

kitaifa na sheria kufafanua ni nani hasa mmiliki wa elimu tamaduni. Mmiliki wa elimu tamaduni anaweza kuwa mtu binafsi, kikundi ama jamii kwa jumla.

Nne, ili kuweza kutimiza kanuni za Ufikiaji na Ugavi wa Faida zitokanazo na Chembechembe za Biolojia, mpangilio wa kufikia kumbukumbu hizi ni sharti ziwe za kufaa, ikiwemo kupata kibali cha awali kutoka wamiliki kutokana na makubaliano ya wamiliki na washirika. Makubaliano haya yanaweza kufuata desturi za wamiliki, bora tu zisiwe zimeenda kinyume na sheria za kitaifa. Changamoto iliyopo hapa ni elimu tamaduni ambayo inajulikana na kumilikiwa na jamii kadhaa. Je ni jamii gani ina haki ya kupewa kibali cha mali miliki na kuingia makubaliano ya Ufikiaji na Ugavi wa Faida?

Mwisho, katika jamii nyingi, elimu tamaduni ni siri. Lakini katika jamii nyingi Madagascar, elimu tamaduni haifichwi hasa kama inaenda kusaidia wengine. Kuna haja basi jambo hili kuambatana na kanuni za Ufikiaji na Ugavi wa Faida ili kuepuka mitego inayotoa nafasi za matumizi mabaya ya elimu hii.

Itifaki za Jamii zina umuhimu wa kuweka masharti ya ufikiaji wa

elimu tamaduni kulingana na desturi za jamii na haki za jamii asili zinazotambulika kimataifa. Jambo hili lilitiwa maanani katika mchakato wa kutengeza itifaki za jamii katika maeneo ya Mariano, Analavory na Antavolobe. Kuna jambo linguine tulitilia maanani pia. Rasili mali na elimu inayo ambatana na rasilimali hizi zina uhusiano wa karibu. Jambo hili si



Jamii mashinani wakifundishana kupitia elimu simulizi na kwa vitendo.

la kusahau wakati wa kutengeneza itifaki za jamii.

Kuna njia nyingi zinaweza kubuniwa kulinda elimu tamaduni. Jukumu kubwa ni kuchagua ni njia ipi inafaa zaidi kwa hali zetu, ama kubadilisha mipangilio hii ili kuweza kufaa hali zetu. Lakini kwa vyovyote vile kuna umuhimu wa kuwa na sheria thabiti za kitaifa kama nguzo yetu. Nchi zina uhuru wa kuunganisha sheria za elimu tamaduni kwa sheria zilizoko ama kutengeneza sheria moja ya kitaifa ya Ufikiaji na Ugavi wa Faida za Chembechembe za Biolojia. Njia yoyote ile itakayochaguliwa, ni muhimu kuhususha jamii mashinani. **10**



# Upanzi wa Miti Shambani ni Kilimo Mbadala!

**Bi. Nancy Saumu Ronald ni Afisa wa Misitu anapendekeza kilimo cha miti shambani kukimu mahitaji ya mbao.**



**Kwa kufahamu na kupenda kazi na mambo muhimu ya mazingira.**

Motisha wa kuhifadhi mazingira hutokana na faida nyingi zinazo toka kwa mali asili. Kama afisa wa misitu, jukumu la kuhakikisha mazingira inalindwa ni wito mkubwa kwangu ambao nautekeleza kwa ushirikiano na wengine kupitia uhamasisho na kujenga uwezo wa wadau.

Kuna mambo mawili muhimu ya kutilia maanani kuhusu mazingira. Mazingira safi ni muhimu kwa afya yetu na maendeleo. Lakini la muhimu zaidi ni kwamba mazingira bora huweza kutoa bidhaa na huduma zinazowesha uchumi kukuwa na kuinua maisha ya binadamu. Kuna faida nyingi za misitu, kama vile, ukuzaji na uuzaji wa miche, uuzaji wa bidhaa kadha wa kadha za miti na hivi punde kumekuwa na uuzaji wa hewa mkaa kulingana na uwezo wa miti hai kunasa hewa mkaa.

Upanzi na utunzi wa miti una changamoto zake. Wakuzaji na wasimamizi wa misitu hupata changamoto kama vile: -

- Mabadiliko ya hali ya hewa ambayo huathiri upanzi na ukuzaji wa miti. Athari za mabadiliko ya hali ya hewa zinaweza punguzwa ikiwa tutapunguza uharibifu wa mazingira kwa kupitia njia kadha wa kadha ikiwemo upanzi wa miti na uhifadhi wa misitu tuliyo nayo,
- Uhamasisho wa umma kuweza kuchukua hatua muafaka za kulinda mazingira ni changamoto nyingine. Wengi wetu tunajua umuhimu wa kupanda miti na athari za kuharibu misitu, lakini wachache wetu wanajua njia bora za kupanda na kukuza miti ili tuweze kupata mavuno zaidi kutoka kwa miti,
- Mfumo wetu wa masomo una wingi wa nadharia na uchache wa mazoezi yanayo ambatana na hali halisi. Kuna haja ya masomo kwenda sambamba na teknolojia chipukizi za kilimo cha miti,
- Kuna upungufu mkubwa wa mbao na mahitaji ya mbao yamezidi uzalishaji. Mahitaji ya mbao na bidhaa zake imepelekea watu wengi kutafuta mbinu mbadala ambazo haziwezi dumishwa na zinazo

haribu misitu.

Upanzi wa miti shambani unaonekana kuwa njia mbadala ambayo itapunguza uharibifu wa misitu. Sehemu nyingi za nchi ya Kenya hazifai kwa upanzi wa miti na sehemu chache zilizoko ni za kilimo cha mimea na shughuli zingine za maendeleo. Ikiwa tutaweza kuwarai watu wapande miti kidogo kwa mashamba yao kwa kuanzisha vijishamba vya miti ama upanzi wa miti katika mipaka ya shamba, tutaweza kujaza pengo lililoko la upungufu wa mbao.

Ni muhimu kwa wakulima ambao wako tayari kuanzisha vijishamba vya miti ama kupanda miti shambani kwa ujumla, kufahamu mazingira yao kabla kupanda miti. Kila aina ya mti una mazingira yake ya kuweza kukuwa vizuri. Katika shughuli zangu za kila siku, huwasaidia wakulima kutathmini sehemu za kupanda miti na aina ya miti inayofaa sehemu hizo kabla kuanza shughuli za upanzi wa miti. Shughuli hii huhakikisha kuwa miti inayopandwa inafaa sehemu hiyo. Baada ya kutambua aina ya miti ya kupanda shambani, mkulima anahitaji muongozo wa kutayarisha, kukuza, kuvuna na kutaftia soko miti atakayokuza. Jambo hili husaidia mkulima kuweza kupata mavuno zaidi kutoka kwa miti yake.

Kwa wale wakulima wenye vijishamba vya miti, wanachohitaji ni usaidizi wa mara kwa mara ili kuhakikisha miti inakuzwa vyema. Kuna mambo kadhaa yanayo zingatiwa tukitathmini ukuaji wa miti. Mambo haya ni kama: -

- Kuangalia na kuweka kumbukumbu za aina ya miti inayokuzwa,
- Kukadiria jinsi miti inavyokuwa shambani na kupima kimo, upana na afya ya mti. Habari hizi zinasaidia kutambua ukuaji wa mti ukiwa na nguvu, ukiwa na shida fulani, ukiwa na



### Utathmini wa ubora wa udongo

magonjwa ama kuvamiwa na wadudu,

- Kukadiria ubora wa udongo kwa kuchimba shimo dogo ili kuangalia kwa karibu aina ya udongo shambani. Udongo mzuri lazima uwe na uwezo wa kupitisha maji na kusaidia mizizi kupenya. Udongo dhaifu ni kama vile mchanga na udongo wa mfinyanzi.
- Kukadiria usimamizi wa miti kwa kuhakikisha nafasi ifaayo kati ya miti, kupogoa tagaa zisizofaa, kungoa miti ili kutoa nafasi kwa miti mingine kukua vizuri, na hata kuchunguza vyanzo vya mbegu za miti.

Kuna haja ya kuunga mkono juhudi za kuanzisha na kuendeleza vijishamba vya miti shambani kwa vile ina uwezo wa kupunguza uhaba wa mbao, kuongeza mapato kwa mkulima na pia kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.



# Mseto wa Habari!

## Sauti Muhimu: Mregesho Wako!

### Kukiuka Marufuku ya Plastiki

Wenye maduka na wanabiashara wadogo wadogo Mara wameanza kutumia tena plastiki zilizo pigwa marufuku. Tumeanza kuwahamasisha kuhusu marufuku hiyo na athari zake. Tunahitaji kila mmoja, hasa maafisa wa serikali, kutusaidia ili tufaulu – **Mr. Reuben Soit**, P4N-291, Kaunti ya Narok, Kenya.

### Dunia, Mlezi Wetu

Dunia na mazingira yake ni mlezi wetu, nasi ni watoto wake. Nina wahimiza wenzangu tutunze mazingira na Dunia yetu – **Bw. Amos Kahindi**, P4N-367, Kaunti ya Kilifi, Kenya.

### Nilifurahia Kusoma Toleo la 2

Mimi nilifurahia kusoma toleo la 2 la jarida letu - **Dkt. Stellan Mukhovi**, P4N-311, Kaunti ya Kakamega, Kenya.

Pongezi! – **Bi. Elizabeth Mwambui**, P4N-356, Kaunti ya Taita Taveta, Kenya na **Bw. Sam Maina**, P4N-279, Kaunti ya Nairobi, Kenya.

### Nafasi ya Kupigiwa Simu

Si wote tuna simu za kisasa zinazoweza kutuunganisha na mtandao wa intaneti ama hata hela za kupiga simu. Je mnaweza kuweka siku ama wakati mkapigia simu baadhi yetu kupata mregesho wetu? – **Mr. Amos Kahindi**, P4N-367, Kaunti ya Kilifi, Kenya.

## Mtandao wa Kina Mama

Mjadala wa kuunda mtandao wa kina mama wa P4N ulianza 2014, ukafufuliwa 2017 na 2018. Ofisi ya Katibu iliwatumia wakina mama wa P4N ujumbe mfupi na haya ndiyo walisema:

Kuna haja ya wakina mama mashinani na wakina mama viongozi kushirikiana, kusaidiana na kujifunza kutoka kwa kila mmoja ili waweze kuchangia vilivyo katika usimamizi bora wa mazingira – **Bi. Rashida Zaid**, P4N-290, Arusha, Tanzania.

Ni maoni yangu kuwa mtandao huu ukuze masomo, uhamasisho, kutembeleana, na kadhalika – **Bi. Beatrice Mutahi**, P4N-026, Kaunti ya Nyandarua, Kenya.

Ni wazo zuri sana. Mtandao utawezesha kina mama kuhusishwa vilivyo katika usimamizi wa mazingira. Ni jukumu sasa la kina mama kusukuma agenda hii mbele – **Rev. Jackline Loroghwa**, P4N-111, Taveta, Kenya.

Mtandao huu usitenge wakina baba. Tunaweza wahusisha kama marafiki wa mtandao wetu – **Bi. Nancy Saumu Ronald**, Mshirikishi, Jukwaa la Misitu na Wanyama Pori, Kilifi, Kenya.

Wazo hili limekuja wakati mzuri – **Bi. Catherine Musili**, P4N-348, Mombasa, Kenya.

Muundo wa mtandao huu ungefuata muundo wa Jukwaa la Vijana – **Bi. Phathisani Tabengwa**, Mshirikishi, Jukwaa la Elimu, Bulawayo, Zimbabwe.

## Kadi za Siku ya Kuzaliwa



Tungependa kumjibu **Bi. Mary Mnene**, P4N-172, Kaunti ya Taita Taveta, Kenya, kwamba mpango huu wa kutuma kadi ulianza 2017. Kadi hizi zinatunwa kupitia mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Instagram na WhatsApp. Yeyote anayetaka kujumuishwa katika mpango huu atutumie siku ya kuzaliwa kwake.

## Karibuni Nyumbani!



Tunayo furaha ya kuwakaibisha kwa mtandao wanachama watatu robo hii. **Bi. Anzana Basnet** (kwa picha) anakuwa mwanachama wetu wa tatu kutoka Nepali. Wengine waliojiunga nasi ni **Bibiana Mnawe** (Kaunti ya Taita Taveta, Kenya) na mtoto **Mercy Jumwa Karisa** (Kaunti ya Kilifi, Kenya).

## Wasiliana Nasi!

Barua Pepe: [people4nature@africanature.or.ke](mailto:people4nature@africanature.or.ke),

Ukurasa wa Facebook: People4Nature Global,

Akaunti ya Facebook: Watu Mazingira,

Instagramu: People4Nature,

Twitter: People4Nature Global,

LinkedIn: People4Nature Global,

Tuvuti: [www.africanature.or.ke](http://www.africanature.or.ke)

People4Nature  
 Belong!

SLP 2227, 80100, Mombasa Kenya

Simu 1: +254 717 127 800

Simu 2: +254 780 127 800

Hazina Mazingira: +254 777 127 800